

## VITABU VYA KUTAFSIRIWA NA FASIHI YA KISWAHILI

Charlotte W. Ryanga

Miongoni mwa wana-chuo katika Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi, mlizuka mjadala kuhusu vitabu vilivyotafsiriwa na kukubaliwa kwake katika fasihi ya Kiswahili. Katika mjadala huo ilidaiwa kwamba vitabu vilivyotafsiriwa havina nafasi katika fasihi ya Kiswahili. Dai lingine lilikuwa kwamba tafsiri hizo zinaua fasihi ya Kiswahili badala ya kuiendeleza. Madai haya yote hutolewa kwa sababu wasomi wa tafsiri hizo za fasihi iliyoandikwa asilia kwa lugha nyingine, huwa hawaoni mnato wala ladha yoyote ya kisanaa kwenye kazi hizo. Nyingi ya kazi zilizotafsiriwa lugha yake huwa ya kiwango cha chini. Lugha inayotumika huwa haina ufasaha kama lugha katika tungo asilia. Kwa sababu hii, maudhui ya tafsiri hayaendelezwi vyema au ujumbe unaowasilishwa mara nyingi unapotoka.

Dai jingine linahusu ufunzaji wa uchambuzi wa vitabu vya fasihi vilivyotafsiriwa. Yasemwa kwamba matumizi ya lugha katika hazi hizi hutatanisha wakufunzi pamoja na wakurufunzi. Kwa mfano, kwenye mtaala wa fasihi darasani, mkufunzi anapowaambia wanafunzi wachambue matumizi ya lugha, mtindo, na mbinu za mwandishi hali kitabu kihusikacho kimetafsiriwa, hapo mwanafunzi atakuwa anachambua umbuji wa mtunzi au mfasiri? Hili ndilo jambo linalokanganya.

Kwamba vitabu vya fasihi vilivyotafsiriwa kwa Kiswahili vina dosari ni jambo lisilokanushika. Mambo muhimu yanayojitokeza kama dosari zaidi ni katika upande wa sarufi, matumizi ya lugha na mantiki - yaani ukosefu wa uthabiti katika uwasilishaji wa ujumbe asilia kwenye tafsiri.

Mpaka sasa uchunguzi haujafanywa juu ya kipengele hiki cha tafsiri; uchunguzi ambao ungefichua jinsi mambo

yaliwyo hata kusababisha mjadala wa aina hii miongoni mwa wasomi wa fasihi. Utafiti pia haujafanywa kuhusu mambo yanayosababisha dosari hizo kwenye tafsiri, dosari ambazo zinawaathiri wale wanaokataa kuvikubali vitabu vya tafsiri katika fasihi ya Kiswahili.

Kwanza ni bora kutazama dosari zilizojificha, kiini cha dosari hizo na kuona kama zinaweza kurekebishika. Pili, dosari hizo zichunguzwe ikiwa kwa hakika zina uzani wa kusababisha tafsiri za vitabu vya fasihi zitupiliwe nje ya fasihi ya Kiswahili. Kulingana na hoja zilizo-tangulia, hatuna budi kujiuliza kama inahalisi kuvitweza vitabu vya tafsiri na kuviondoa kwenye fasihi, pasi ya kuzingatia mambo mbalimbali kuhusu jukumu la tafsiri, na matatizo yanayomsibu mfasiri katika kutekeleza kazi yake. Inafaa utafiti ufanywe kufuatia taratibu maalumu hadi kufikia maafikiano ya kuzikataa ama kuzikubali tafsiri katika fasihi. Bila kufanya hivyo, hoja na madai ya wapinzani hayatakuwa na msingi.

Kabla ya kujadili hoja zilizotangulia yafaa, tuzungumzie kwa muhtasari mambo mawili muhimu: kwanza ni jukumu la fasihi, pili ni jukumu la tafsiri. Fasihi hujishughulisha na taratibu za jumuiya. Fasihi ni kazi ya sanaa inayochukua jukumu la kutudhihirishia na pengine kututatulia hali zetu za kisiasa, kijamii, na kiutamaduni kwa jumla. Ni yakini kuwa fasihi ni mdhihirisho ama kioo cha maisha ya jamii na uhusiano wao katika muktadha wa mazingira na maumbile yao. Hivyo fasihi inafunza na kutumbuiza. Maelezo haya yanamaanisha kwamba maendeleo ya fasihi hayana budi kuzingatiwa ku-ambatana na mujibu wa maendeleo ya jumuiya yenyewe na utamaduni wake. Moja kati ya sifa za fasihi ni matumizi mazuri ya lugha. Neno "fasihi" limetokana na ufasaha wa lugha. Ufasaha wa lugha huendeleza umbuji wa mwandishi kwa kutiririsha kadhia zake vizuri. Ikiwa lugha si sahihi, basi sanaa ya fasihi haitapendeza kimantiki, ki-lugha na hata kisanaa.

Jukumu la tafsiri nalo limeambatana sana na lile la fasihi. Tafsiri ina madhumuni ya kuwasilisha ujumbe wa manufaa kwa watu ambao hawafahamu lugha asilia iliyotumika kwenye maandishi yanayohusika. Hivyo tafsiri pia inatambulikana kama kazi ya kisanaa mithili ya sanaa ya fasihi, kuchora ama kuchonga sanamu. Sanaa ni kipawa cha mtu binafsi. Watu wote hawana kipawa kimoja tu, bali wana vipawa tofauti; wengine huchora picha, wengine hu-

jenga na kadhalika. Baadhi ya watu wanaweza kuzimudu sanaa kadha wakati mmoja, lakini si kazi rahisi.

Tukidai kwamba vitabu vya fasihi vilivyotafsiriwa vikubaliwe katika fasihi ya Kiswahili inatupasa kuzingatia shuruti zake ambazo lazima zitimizwe kabla ya kutekeleza mujibu huu. Kuna sifa nne ambazo mfasiri shurti awe nazo:

1. Ufahamu mkamilifu wa ujumbe asilia na jinsi ya kueleza katika lugha pokezi.
2. Umahiri na hisi za kisanaa.
3. Ujuzi wa lugha fasaha - lugha pokezi na lugha asilia.
4. Ufundi katika mbinu na taratibu za sanaa hii, na pia somo analolitafsiri.

Vitabu vya tafsiri pamoja na tungo asilia za fasihi vinatumika na kusomwa na watu wengi sana. Hivyo kila mfasiri hana budi kuzingatia jambo hili ajitokeze na kazi za kisanaa zisizotweza taaluma hizo wala kuaibisha lugha iliyotumika. Tuzingatiapo haya yote ndipo inapotuhalisisi kujipurukusha na kusuluhisha mjadala huu kwa ajili ya kuleta maafikiano baina ya wana-fasihi na wana-tafsiri.

Katika kuamua ukubalifu wa vitabu vya tafsiri katika fasihi shuruti tujiulize kama vitabu vilivyotafsiriwa vinakidhi dhima ya fasihi ya Kiswahili. Utafiti katika mitaala ya fasihi ulimwenguni umedhihirisha kutumiwa kwa vitabu vya tafsiri katika fasihi ya lugha nyingine, iwe ni fasihi ya Kiingereza, Kirusi, Kifaransa na kadhalika. Kwa hivyo matumizi ya tafsiri katika fasihi si jambo geni. Ikiwa fasihi ya Kiingereza na Kifaransa imeruhusu tafsiri za lugha nyingine zitumike katika somo la fasihi yao, (kwa mfano Odessey na Iliad, vitabu vilivyotungwa asilia kwa Kigiriki, The Government Inspector, ambacho kiliandikwa asilia kwa Kirusi, The Plague, The Houseboy, n.k. vilivyotafsiriwa kutoka Kifaransa), sioni ni kwa nini hatua hii ikataliwe kwenye fasihi ya Kiswahili. Kukataliwa kwake bila shaka kunasababishwa na mambo mengine yaliyomo katika tafsiri zenyewe wala siyo katika ile dhana ya tafsiri peke yake.

Vitabu vya fasihi ya lugha ngeni vinapotafsiriwa huendeleza jukumu la fasihi na kupanua maudhui yake katika



ile lugha pokezi; maudhui kama ya kiijtimai, ya ku-furahisha, ama kadhia mbalimbali juu ya maslahi ya jumuiya nzima. Ikiwa vitabu hivyo havikidhi haja au dhima ya fasihi kama ilivyokusudiwa katika lugha pokezi, basi itakuwa sawa kuvizulia visitumiwe katika soko la fasihi la lugha inayohusika.

Sababu ya lugha nyinginezo kukubali vitabu vya tafsiri ni kwamba tafsiri hizo husaidia kupanua mawazo na fikira za wasomaji pamoja na jamii ya waandishi - kimtindo, kimaudhui, kiumbuji n.k. Kazi ya tafsiri hupanua ujuzi wa kisanaa, na kuwaelimisha wasomaji juu ya maisha ya watu wanaoishi katika mataifa na tamaduni nyinginezo. Tena tafsiri hazipanui mawazo tu bali huwapa waandishi fikira mpya, uvumbuzi wa mbinu mpya za kisanaa na kuwaathiri na kuwashawishi kufanya majaribio ya mbinu ngeni katika maandishi yao wakitumia lugha yao wenyewe. Hii ni faida inayoongeza hazina ya elimu katika kuzijua jumuiya mbalimbali, na kuzilinganisha na zetu ili kukadiria maendeleo tunayoyatarajia kisiasa, kijamii na kielimu. Hili pia ni jukumu la fasihi.

Matumizi ya vitabu vilivyotafsiriwa kwenye fasihi ya Kiswahili hayakuanza sasa kufikiriwa. Ushirikiano huo ulikuweco tangu zamani. Kwa hivyo pengine mjadala unge-elekea upande wa "kuondolewa kwa vitabu vya tafsiri katika fasihi ya Kiswahili" wala siyo, "kukubaliwa kwa vitabu vya tafsiri katika fasihi ya Kiswahili." Ninasema hivi kwa sababu tunapochunguza maandishi ya fasihi ya Kiswahili, itaonekana wazi kwamba vitabu vya tafsiri vilikuwa vikitumika tangu zamani, ambapo fasihi kwa lugha ya Kiswahili ilikuwa haijaendelea sana.

Baadhi ya tafsiri zilizokuwa zikitumika tangu zamani ni: Hekaya za Abunuwasi, Alfu-lela-Ulela, Elisi Katika Nchi ya Ajabu na vitabu vinginevyo. Baada ya muda, baadhi ya waandishi kwa lugha ya Kiswahili waliathiriwa na fasihi hiyo. Athari hizi zadhihirika katika hadithi zilizobuniwa na waandishi chipukizi wa Kiswahili kama mwandishi maarufu Shaaban Robert: Kusadikika, Adili na Nduguze; halafu Kurwa na Doto, (M.S. Farsy); Nahodha Fikirini, (Ali Jamadaar); Kisima cha Giningi, (Mohamed S. Abdulla). Si ajabu basi kuona siku hizi vitabu vya tafsiri vikienea na kuathiri fasihi ya Kiswahili kila upande - tamthlia, riwaya na hata ushairi (arudhi za ushairi wa Kiswahili zaonyesha athari za kigeni). Tafsiri kama Mabepari wa Venisi, Juliasi Kaizari, Mfalme

Edipode, na Wema Hawajazaliwa, zinazotokana na mataifa mengine barani Afrika na Ulaya; zinatekeleza jukumu la kuijenga fasihi ya lugha inayofanyiwa tafsiri na kupanua daraja yake kisanaa na kitamaduni.

Sababu mojawapo ya kuenea kwa vitabu vya tafsiri kwenye fasihi ya Kiswahili ni upungufu wa vitabu vya tungo asilia ambazo zinatoshuleza wadhifa wa fasihi kikamilifu. Twasema haya hasa tunapofikiria kiwango cha maandishi ya fasihi ya Kiswahili katika Afrika ya Mashariki - kimaudhui au kifasaha - kiwango ambacho kitakidhi watu wa daraja mbali mbali za mtaala huo. Ni dhahiri basi kwamba kuwako kwa vitabu vilivyotafsiriwa kama ziada ya vitabu vya fasihi ni jambo la maslahi, na maendeleo ya fasihi kwa jumla. Hivi tunakubaliana na maoni ya Kazungu na Mazrui yanayosema:

kwa bahati mbaya watu wengi leo wanazikataa tafsiri hizi na kudai kuwa haziingii katika fasihi ya Kiswahili. Lakini endapo tafsiri hizi zimetumia lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa mbinu zake za kifasaha, basi kitendo cha kuzitoa katika fungu la fasihi ya Kiswahili kitakuwa ni cha taasubi tu kisichokuwa na mantiki yoyote.

Hebu sasa tujaribu kuchambua kwa ufupi maudhui machache yaendelezayo fasihi ya Kiswahili kama ilivyo leo katika nyanja za riwaya na tamthlia. Ili kutekeleza uchambuzi huu sawia, yafaa tuigawe fasihi katika mafungu matatu:

1. Fasihi wakati wa ukoloni
2. Fasihi baada ya uhuru
3. Fasihi juu ya ukoloni mamboleo.

Wakati wa ukoloni, maudhui ya tungo asilia yalielekea zaidi katika upande wa kufurahisha - katika riwaya na tamthlia. Kwa mfano, Nakupenda Lakini;... ni mchezo unaotongoa maisha ya kijamii, lakini maudhui yake si mazito hayazungumzii mambo kama kujitafiti, uzandiki na mengineyo. Hali kadhalika, ziko tafsiri zilizofanywa kutoka lugha nyingine kama Kiingereza - Elisi Katika Nchi ya Ajabu; na kutoka Kiarabu kama, Hekaya za Abunuwasi. Maudhui ya tafsiri hizi ni ya

kuwafurahisha wasomi walioandikiwa, - kuwapatia watu fursa ya kusoma ... isiyohitaji uzito wa fikira kwa kuyaelewa yanayoendelezwa vitabuni humo.

Baadhi ya vitabu vilivyofasiriwa siku hizo, vinaonyesha maudhui yanayowatwaza wazungu, kuonyesha ustaarabu na uwezo wao, huku wakiwatweza Waafrika na kuwaonyesha uduni wao. Maudhui haya yanapatikana kwenye tafsiri kama vile Mashimo ya Mfalme Suleiman.

Fasihi baada ya uhuru ilifuata mkondo wa kuonyesha ubovu na udhalimu wa wakoloni. Waandishi asilia katika lugha ya Kiswahili walijitosa katika lindi la kuonyesha mwamko wa Waafrika katika kuutetea na kuupata ukombozi wao, huku wakionyesha kila aina ya uonevu waliofanyiwa na wakoloni. Mfano ni waandishi kama Ebrahim Hussein katika Kinjeketile na Mugyabuso Mulokozi, katika Mukwava wa Uhehe. Tafsiri ziendelezazo maudhui haya pia zilichipuka: kwa mfano, Mchimba Madini na Boi.

Kundi la tatu lina maandishi asilia na tafsiri pia. Tasnifu za vitabu hivi zaidi ni juu ya ukoloni mamboleo, unyanyasaji wake, mifumo ya kisiasa na sera za jamii katika nchi zilizojiipatia uhuru. Baadhi ya vitabu vya tungo hizi za fasihi ni Mashetani (E Hussein); Nyota ya Rehema (S.M. Mohamed) na Asali Chungu (S.A. Mohamed) n.k. Tafsiri zinazojidhihirisha na maudhui haya ni kama vile Mkaguzi Mkuu wa Serikali (Nikolai Gogol). Tamthilia hii ilitafsiriwa kwa Kiswahili kutokana na chapa ya Kiingereza ambayo pia ilitafsiriwa kutoka katika Kirusi ambayo ndiyo lugha ya tungo asilia. Tafsiri nyingine ni kama: Mabepari wa Venisi na Juliasi Kaizari, tungo za William Shakespeare zilizotafsiriwa na Mwalimu J. Nyerere; Wema Hawajazaliwa cha Ayi Kwei Armah, kilichotafsiriwa na Abdilatif Abdallah kutokana na tafsiri ya Kiingereza.

Maudhui ya vitabu hivi vya tafsiri hueleza tabia mbalimbali za kijamii zinazoendelea katika mataifa na tamaduni nyinginezo. Hii hutupa nafasi ya kujichunguza na kupanua mawazo ya jamii zetu katika mazingira yetu. Licha ya hivyo, hata tunapochambua uketo wa tafasiri hizo, tunaonyeshwa uzandiki, ufisadi na ubwanyenye. Kwa ufupi tunadhihirishiwa uonevu uliojikita katika jamii ya kila nchi, - hali ambayo inapatikana miongoni mwa jumuiya nyingi za nchi huru za Afrika. Uketo huo pia unajitokeza katika tungo za Kiswahili zisizokuwa tafsiri. Wasomi wa fasihi asilia pamoja na tafsiri wanapata kuelimishwa na



kuweza kuona hali ya jumuiya ya kisiasa na kijamii katika muktadha wa Bara zima la Afrika, na hata kwingineko ulimwenguni. Jambo hili linatudhihirishia kwamba tabia za maisha ya jamii mbalimbali zimejikita katika nafsi za binadamu wote bila kuzingatia nchi zilizowalea iwe ni Uzunguni, Arabuni, Merikani ama Afrika.

Vitabu vingi vya fasihi, tafsiri na tungo asilia vinaonyesha jinsi watu wanavyokata tamaa, jinsi wanavyoona uongozi wa nchi zao ima ukijikita kwenye mataribushi ya wakoloni au kuzusha dhuluma mpya za viongozi za kuwanyanyasa wazalendo wenzao. Ubinafsi hapa unajitokeza. Ayi Kwei Armah katika kitabu chake Wema Hawajazaliwa, anaonyesha kukata tamaa kwa raia juu ya uongozi wa serikali yao mpya baada ya mapinduzi. Ebrahim Hussein, kwenye Mashetani anaonyesha jinsi mabwana wapya wanavyochukua mahali pa wakoloni - kwa sababu ya athari za kigeni. M.S. Mohamed katika Nyota ya Rehema anaonyesha jinsi Waafrika wenye vyeo wanavyowadhulumu wengine wasiopata kubahatika maishani mwao. Mifano hii yadhihirisha kwa nini tukasema vitabu vilivyotafsiriwa vinaweza kuiteleza fasihi ya lugha ambayo inafanyiwa tafsiri.

Katika kujadili swala hili, isidhaniwe kwamba tunatetea kazi za tafsiri bila ya kuzikosoa. La. Kwamba tafsiri nyingi za Kiswahili zina dosari ni kweli isiyo-pingika. Dosari zenyewe zinajitokeza katika sehemu za uthabiti - kuhifadhiwa kikamilifu kwa ujumbe asilia kwenye tafsiri; na upande wa ufasaha wa lugha.

Malalamiko mengi kuhusu undani wa vitabu vya tafsiri ni pamoja na kusema kuwa havina lugha fasaha yenye ladha, mtiririko wala msamiati ufaao. Yasemwa pia kwamba tafsiri hazina uthabiti katika ujumbe uwasilishwao; ama zinaacha mambo mengine nje ya tafsiri au huwa na ziada ya maoni ya kibinafsi na hisi ambazo hazikudhamiriwa na mwandishi asilia.

Ni kweli kwamba kazi nyingi za tafsiri zina dosari hizo mbili. Mara nyingi mambo hayo hutokea pasi na mfasiri mwenyewe kujua. Lakini, wakati mwingine haya hutokana na juhudi za mfasiri kujaribu kufafanua ujumbe wa mtunzi. Katika kujitahidi kufanya ufafanuzi huo mfasiri huweza kuacha vifungu anavyoviona vigumu kuvieleza kwa usahihi katika lugha anayoifanyia tafsiri. Jambo la kusema hapa ni kuwa ingewapasa watu wenye maoni haya kwanza wazingatie masharti na matatizo yanayoambatana na kazi ya kutafsiri.

Kwa sababu tafsiri kuhusu kazi ambayo imekwisha kutungwa na msanii mwingine si ajabu kusema kwamba daima kutakuwa na tofauti baina ya aina hizo mbili za maandishi. Hata hivyo tofauti hii si lazima iegemea kwenye upande wa tafsiri mbaya. Kama vile ambavyo tungo asilia zisifiwazo kwenye fasihi hutegemea uzuri na ufasaha wa matumizi ya lugha, pamoja na mbinu za kisanaa (siyo maelezo ya kadhia tu), vilevile tafsiri hutegemea mambo hayo. Kama vile ambavyo mtunzi akikosa kuimudu lugha kwa ufasaha katika sanaa yake wasomaji wake huyaona maandishi yake yakichosha, ndivyo pia ilivyo kwa mfasiri. Wasifu wa tafsiri kama kazi nyingine za kisanaa unatokana na utamu wa mdundo wa lugha iliyotumiwa, mfululizo wa taswira na jazanda zikubalikazo katika lugha pokezi, mtiririko wa kadhia na uhifadhi wa ujumbe. Inatupasa kufahamu kuwa uthabiti kwenye tafsiri ndio unaowapendeza wasomaji.

Sasa na tutazame mfasiri na matatizo yanayomsibu katika kazi yake. Tatizo la kwanza ni lile jukumu la kusoma maandishi asilia ya lugha nyingine hadi ayafahamu kinagaubaga halafu aweze kuyafikiria katika lugha ya tafsiri. Yapasa kufahamu pia muktadha wa maandishi hayo asilia ili aweze kuielewa lugha ya mwandishi - afahamu kama mwandishi ametumia lugha nzito yenye hisia, au lugha nyepesi isiyo-hitaji fikira za msomaji. Pili, mara nyingi lugha asilia pamoja na ile ya tafsiri huwa zote ni lugha za kujifunza za mfasiri - hapana moja ambayo ni lugha yake ya malezi - hivyo ni lazima awe na ujuzi mzuri wa lugha zote mbili ama sivyo, vikwazo vitatokea katika ufanyaji kazi hiyo. Haya ni kinyume cha mtunzi asilia. Maudhui ya mwandishi asilia anayoyaandika ni yake binafsi, yeye ndiye aliyeyaibua; ndiye aliyeyaunda kwa dhamira yake na wala hana haja ya kuyaambatanisha na mawazo ya mtu mwingine. Pia ujuzi wa lugha unaohitajika ni ule wa lugha moja aliyochagua kuitumia kwa kuandika kadhia zake. Lakini hata katika vitabu vilivyotungwa asilia pia huwa kuna dosari kwa kiasi fulani. Sasa ikiwa mtungaji asilia huweza kuona ugumu na kughafilika katika matumizi ya lugha fasaha si ajabu kwa mfasiri anayehitajika kufikiria katika lugha mbili wakati anapofanya kazi yake kuwa na dosari.

Tatizo jingine kwa mfasiri linahusu msamiati ambao utaweza kuwasilisha maudhui ya mwandishi katika uzito au wepesi wake, msamiati ambao utawaridhisha wasomi wa tafsiri kama vile maandishi asilia yanavyowaridhisha wasomaji wake. Utatuzi wa tatizo hili unategemea umahiri wa mfasiri katika mbinu za utekelezaji wa tafsiri. Ugumu



hutokea iwapo misemo au maneno mengine hayaelezeki kirahisi katika lugha ya tafsiri ama kwa sababu dhana za misemo hiyo ni ngeni katika lugha pokezi, au pengine tafsiri zilinganazo na dhana hizo za lugha asilia hazi- pendezi zikitumika katika lugha nyingine.

Mfasiri mweledi lazima awe na lugha yenye mdundo, inayoeleweka kinaganaga, aweze kujenga kadhia za tungo asilia vizuri pasi na kuzungukazunguka. Haya yote yatekelezwapo tafsiri itaonekana nzuri na yenye kuwa- pendeza wasomaji. Ni kutokana na hali kama hii tunapo- ona kwamba tafsiri zinazofanywa kwa Kiingereza kutoka lugha nyinginezo kama vile; The Plague (Camus); Crime and Punishment (Leon Dostoevski) zilitungwa asilia kwa Kifaransa na Kirusi zinazosomeka na kupendeza kama tungo asilia. Si rahisi kwa msomaji kutambua kuwa hizi ni tafsiri. Labda swali la kujiuliza kwa nini tafsiri za Kiswahili haziwi hivyo.

Yafaa tujue kuwa wale wanaofanya tafsiri za Kiingereza, huwa watu waliofuzu katika mbinu za taaluma hii ya tafsiri. Wao huwa weledi wa kazi yao. Ni kawaida kuwa kila mfasiri huichukua sanaa hii kama hazi yake maalumu, na hutafsiri makala ya somo analolifahamu sawa- sawa. Baadhi ya wafasiri wa vitabu vya fasihi huwa ni wana-fasihi na wanajua matarajio ya wasomi wa mtaala huo. Pia wafasiri hao hupata msaada wa makamusi na orodha za maneno ya somo walifanyialo kazi, maneno ambayo yameelezwa maana zake mbali mbali, makamusi ya visawe (synonyms), na makamusi yenye kueleza jinsi maneno hayo yanavyotumiwa katika sentensi ama muktadha upasao, mifano mizuri ni kamusi la The Pan Dictionary of Synonyms and Antonyms, lililohaririwa na Laurence Urdang and Martin Manser (1978) na The Concise Oxford Dictionary of Current English lililohaririwa na Fowler, N.W. na Fowler, F.G. Zaidi ya hayo, wanayo makamusi yanayoelezea maana kwa lugha mbili - mfano kamusi ya Kiingereza na Kihispania na la Kihispania - Kiingereza.

Wafasiri wa Kiingereza wengi huhojiwa kwanza kabla ya kuajiriwa ili kuhakikisha kwamba wana sifa zinazo- mstahilia mfasiri. Wafasiri wa namna hii aghalabu huwa na ujuzi mzuri wa lugha zote mbili. Kwa sababu hii tafsiri zilizofanywa kwa Kiingereza hutokea kuwa nzuri. Kwa sasa wale wanaotafsiri kwa lugha ya Kiswahili hali yao na jinsi wanavyofanya kazi ni tofauti kwa ajili ya uchanga wa taaluma hii katika Afrika Mashariki. Ni dhahiri kwamba

vitabu vya Kiswahili vilivyotafsiriwa na wageni - ima Wazungu au Waarabu, kama vile Mashimo ya Mfalme Suleiman na Alfu Lela Ulela, vinasomeka vyema, na vina lugha ya mtiririko kuliko vitabu vinavyotafasiriwa na watumiaji wa Kiswahili humu Afrika Mashariki. Wawe ni watu waliozaliwa uswahilini (Abdilatif Abdalla na tafasiri yake Wema Hawaja-zaliwa) au ni wafasiri waliojifunza Kiswahili baadaye (Christon Mwakasaka na tafasiri yake Mkaguzi Mkuu wa Serikali). Sababu mojawapo muhimu ni kuwa uwanda huu wa tafasiri haujatiliwa maanani hapa Afrika ya Mashariki. Tatizo letu moja ni kwamba mtu yeyote azungumzaye Kiswahili na Kiingereza hujiona tayari anaweza kutafsiri makala yanayohusu lugha hizo. Kwa hali kama hiyo utakuta kwamba watu wasio weledi katika sanaa ya tafasiri, wasio-zijua kanuni na taratibu za tafasiri hujiingiza katika kufanya kazi hii na matokeo yake ni kuvitweza vitabu vya tafasiri kiasi cha kutatanisha ukubalifu wake katika fasihi ya Kiswahili. Haya huja kwa sababu wafasiri wasio-zijua kikamilifu mbinu za taaluma hii, hutafsiri kibubu bila kuzingatia sharti la lahani nyororo na lugha aali katika lugha pokezi.

Yamkinika kwamba wasomi wengi wa fasihi ya Kiswahili hawakatai fasihi iliyotafsiriwa bali wanalopinga ni hali mbaya ya tafasiri zenyewe. Malalamiko yao ni halali kwani hadi leo, kuna tafasiri chache tu miongoni mwao zikiwa za Mwalimu Julius Nyerere kama vile, Juliasi Kaizari, na ya Samuel Mushi - Mfalme Edipode, ambazo ukizisoma zina-ridhisha, kwamba zimetekeleza mbinu ali ali za tafasiri na kuendeleza maudhui asilia kwa lugha fasaha ya Kiswahili.

Wafasiri wa lugha ya Kiswahili hawajapata mwongozo ufaao katika mambo ya tafasiri. Licha ya kutojua undani wa taaluma, hata vifaa vya kuwasaidia pia ni haba. Yako makamusi machache sana ya Kiswahili ambayo yana msamiati utoshelezao. Isipokuwa kwa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) hakuna kamusi jingine la Kiswahili peke yake na ambalo lapatikana kwa urahisi. Yapo makamusi ya lugha mbili. Kiswahili/Kiingereza na Kiingereza/Kiswahili yaliyotungwa na Frederick Johnson. Ukweli ni kwamba makamusi haya yalitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1939 na yaliendelea kurudiwa kuchapishwa mara kwa mara kufikia mwaka wa 1973 bila kubadilisha maneno wala maana zake. Sote hapa tutakubaliana kwamba Kiswahili kilichotumika mwaka huo wa 1973 kilikuwa si toshelezi kwa upande wa ufundi na taaluma mpya mpya. Tunalosema hapa ni kwamba, tangu wakati huo hadi sasa Kiswahili kimekua sana.

Lugha ya Kiswahili imepata mapanuzi ya haraka nchini Kenya tangu 1974 ambapo Kiswahili kilipitishwa kuwa lugha ya taifa na lugha ya mijadala bungeni. Tanzania pia Kiswahili kilihimizwa na kukuzwa ili kitumiwe katika shule kama lugha ya kufundishia, licha ya kuwa cha matumizi ya jumuiya. Kutokana na hali kama hii ni dhahiri kwamba makamusi ya Johnson F. yamepitwa na wakati.

Kuna jambo muhimu ambalo lazima tulitaje hapa, nalo linahusu uhariri na uhakiki wa vitabu vilivyotafsiriwa kwa Kiswahili kabla ya uchapishaji. Wengi kati ya wachapishaji wa vitabu vya tafsiri hawaonekani kuisisitiza uhakiki na uhariri wa tafsiri hizo bali huzichapisha baada ya kuzipitia juujuu kama vitabu vya tungo asilia. Na kama wahariri wanayashughulikia makala ya tafsiri basi pengine hawayahariri wakiyafananisha na makala asilia kama inavyompasa mhariri wa tafsiri kufanya. Haihalisi kuhariri - tafsiri bila kutazama makala asilia. Mhariri anapohariri tafsiri, hasa vitabu vya fasihi, anatakikana kuchunguza mtindo wa mfasiri, matumizi aali ya lugha, kuhifadhiwa kwa kiini cha hadithi na mwendelezo wake sahihi; pia kutazama ikiwa tafsiri inatoa mafunzo ya fasihi yanayotazamiwa kwa wasomaji wa lugha pokezi. Upungufu wa kazi ya wahariri huleta dosari kwa sababu mtindo wa kuhariri kijuujuu hauondoshi makosa wala kuhakikisha kwamba maana asilia imehifadhiwa. Uhariri usiothabiti ndio uzaao vitabu vinavyotatanisha ujumbe na mtiririko wa lugha kwa jumla. Jambo hili huivisha ila sanaa yote ya tafsiri. Matokeo yake tunapata wasomi wa umbuji (Aesthetics) wakisema kuwa kazi za fasihi haziwezi kutafsiriwa. Hawa wanadai kuwa sanaa ya usemi inahusu uchaguzi maalumu na mpango fulani wa msamiati katika sentensi.

Kutokana na yote tuliyoyajadili, msimamo sahihi sasa ni kukubali kwamba vitabu vya tafsiri za Kiswahili huweza kuwa na dosari kwa sababu, tafsiri si kazi asilia na pengine mfasiri hana tajriba ya somo analolitafsiri, tukiacha kando weledi na hisi za kisanaa. Lakini, yote yanapozingatiwa kwa pamoja, hoja hizi haziwezi kufanya vitabu vya tafasiri vikataliwe kwenye fasihi ya Kiswahili. Kinachotakiwa ni sisi wasomaji, wahariri, na wenye kutafsiri kuchunguza na kutafuta njia za kurekebisha dosari zijitokezazo humo. Hili linawezekana.

Utimilifu wa baadhi ya vitabu vya tafsiri na uthabiti wake unapinga maoni ya wasomi fulani wanaodai kwamba Kiswahili hakijitoshelezi kimsamiati - kwa minajili



ya kuendeleza fikira ngeni. Ziko tafsiri nzuri za lugha ngeni kwa Kiswahili. Hoja hii inathibitisha jinsi msamiati wa Kiswahili unavyojengeka, na kuongezeka ambapo bila ongezeko hilo, ingekuwa vigumu kueleza habari na fani mbalimbali za lugha nyingine kwa uthabiti, ukamilifu na ufasaha wa lugha ya Kiswahili. Mwisho tungesema kuwa hakuna ithibati yoyote kuwa kazi za tafsiri haziwezi kuingizwa kisahih katika fasihi ya Kiswahili. Na ikiwa wapo watu ambao bado wangependa kuendelea kuvitweza vitabu vya tafsiri, basi kwanza wangejaribu kuzingatia matatizo yanayowakabili wafasiri. Ni baada ya kuzingatia hayo ambapo tutafahamu sababu zilizomfanya mfasiri Mwalimu Julius Nyerere katika kazi yake Juliasi Kaizari (Utangulizi wa toleo la pili, uk. vi) kusema:

Nimechukua nafasi ya mabadiliko haya pia kusahihisha makosa fulani yaliyokuwamo katika toleo la kwanza. Makosa haya yalikuwa ya aina mbali mbali. Pengine nilikuwa nimekosea tafsiri yenyewe; pengine mistari fulani ilikuwa imeachwa; na pengine kulikuwa na makosa ya kupiga chapa....

Hivyo madai ya kukataa vitabu vilivyotafsiriwa kwenye fasihi ya Kiswahili yaonyesha dhahiri kwamba wenye fikra hizo wana nia ya kuitekuwa kwa tindo na mitaimbo taaluma na sanaa ya tafsiri.

#### MAPENDEKEZO

1. Kuwe na mafunzo maalumu ya wanaotaka kujiunga na kazi za kutafsiri ili waweze kufunzwa taratibu na kanuni za tafsiri kwa jumla, ili kila mtu asijione yu tayari kutafsiri bila kujipatia ujuzi huo. Masomo haya pia yamruhusu mfasiri kujifunza mbinu za somo atakalolifanyia kazi iwe ni fasihi, makala ya sayansi, sheria n.k.
2. Kuwe na wahariri na wahakiki maalumu wa kazi za tafsiri za masomo wanayoyamudu peke yake. Hivi vitazuia uchapishaji wa tafsiri zenye kiwango cha chini katika ukamilifu wake.
3. Mtaala wa tafsiri unahitaji kutiliwa msisitizo katika mafunzo ya lugha kwenye ratiba za shule za

sekondari na hata vyo vikuu. Hatua hii itawafanya watu watilie maanani somo hilo na hivyo kuifikiria taaluma ya tafsiri kama taaluma inayohitaji ujuzi maalumu kama kazi za sanaa nyinginezo.

#### MAELEZO

Lugha pokezi	-	Receptor/target language
Lugha asilia	-	Source language

#### MAREJEO YA VITABU JUU YA TAFSIRI

- Achilles, F. "Some reflections on the difficulty of Translation." In Brower, R.A. On Translation Oxford University Press. New York 1966.
- Ali, C.W. The Problems of Translating From English into Swahili: As Exemplified by V.O.K. News Items. (M.A. Dissertation - Unpublished, U.O.N. 1981).
- Ali, C.W. "Nadharia ya Tafsiri na Mbinu Zake" (Unpublished manuscript)
- Chatman, S. (ed.) Literary Style - A symposium. Oxford University Press, London 1971.
- Harris, L. "Translating Classical Literature into Swahili." In Allen J.W.T. (ed.) Swahili Journal 37-46, 1967/76.
- Hyder, M. "Swahili in a Technical Age" In Africa Contemporary Monographs. No. 4. East African Publishing House. 1966.
- Nida, E.A. Towards a Science of Translating. Netherlands, 1964.
- Ullmann, S. Words and their Use. London, Muller 1951. (Man and Society Series).
- Yaa, J.D. A Guide to English/Kiswahili Translation. Comb Books. Nairobi - Kenya, 1975.
- #### MAREJEO YA TAFSIRI NA TUNGO ZA FASIHI
- Ayi Kwei Armah: Wema Hawajazaliwa, Kimetafsiriwa na Abdilatif Abdalla.

Ferdinand Oyono: Boi Kimetafsiriwa na Raphael Kahaso na Nathan Mwele.

William Shakespeare: Juliasi Kaizari. Kimetafsiriwa na Julius K. Nyerere.

Mabepari wa Venisi. Kimetafsiriwa na Samuel S. Mushi.

Nikolai Gogol: Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kimetafsiriwa na Christian Mwakasaka.

Homer Iliad (Utenzi)

Odyssey (Utenzi)

Lavis Carrol: Elisi katika Nchi ya Ajabu

(Unknown) Hekaya za Abunuwasi. Kilitafsiriwa na The Interterritorial Language Committee, E. Africa.

Robert Louis Stevenson: Kisiwa Chenye Hazina

(Unknown) Alfu Lela Ulela. Kilitafsiriwa na Sir Richard Burton kutoka Kiarabu hadi Kiingereza.

Sir Rider Haggard: Mashimo ya Mfalme Suleiman

Henry Kuria: Nakupenda Lakini....

Said A. Mohamed: Asali Chungu

Ebrahim Hussein: Kinjeketile Oxford University Press.

Mashetani Oxford University Press.

Peter Abrahams: Mchimba Madini

## MAKAMUSI

A Standard English-Swahili Dictionary by the late Frederick Johnson.

A Standard Swahili-English Dictionary by the late Frederick Johnson 1973 (later edition).

The Pan Dictionary of Synonyms and Antonyms. (eds.) Laurence Urdang and Martin Manser.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam. (1981)